***FOMU PLUPA L-2*** ***(r.10)***

## JAMHURI YA KENYA
## SHERIA YA MPANGO WA MIJI NA MATUMIZI YA ARDHI (*Nambari* 13 *ya* 2019)

## ILANI KUHUSU KUKAMILISHWA KWA MPANGO WA USTAWISHAJI

Kichwa cha Mpango wa Ustawishaji: **Mahala patakajengwa Nyumba za Gharama Nafuu, Machakos-Kambi ya Wizara ya Ujenzi Nambari ya PDP: NRB/56/25/01**

**ILANI** inatolewa kwamba, kwa mujibu wa Sehemu ya 13 (g) na 69(1 na 4) na Sheria ya Mpango wa Miji na Matumizi ya Ardhi, 2019 ikisomwa pamoja na Notisi ya Kisheria Nambari 27 ya 2020, utayarishaji wa mpango uliotajwa hapo juu ulikamilika mnamo Februari 3, 2025. Mpango huo wa Ustawishaji unahusu eneo lililoko Machakos Mjini, Kaunti ya Machakos. Nakala za Mpango wa Ustawishaji ulivyotayarishwa umehifadhiliwa kwa ukaguzi wa umma, bila malipo, katika afisi za **Kamishna wa Kaunti ya Machakosa, Waziri wa Kaunti Anayesimamia Idara ya Mpango wa Miji na Matumizi ya Ardhi –Kaunti ya Machakos** na **Mkurugenzi wa Kitaifa wa Idara ya Mpango wa Miji –orofa ya 5, Jumba la Ardhi House, Nairobi; kati ya saa mbili za asubuhi na saa kumi na moja jioni, kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa.** Mtu yeyote mwenye haja ambaye angetaka kutoa maoni au pingamizi kuhusu mpango wa Ustawishaji uliotajwa hapo juu anaweza kuyatuma, kwa maandishi, ili yaweze kupokelewa na Mkurugenzi wa Kitaifa wa Idara ya Mpango wa Miji barabara ya 1st Ngong' Avenue, Jumba la Ardhi House, S.L.P. 45025-00100, Nairobi au kwa njia ya mtandao kwa anwani ya barua pepe : ndpp@ardhi.go.ke ndani ya siku 60 baada ya kuchapishwa kwa notisi hii. Na maoni au pingamizi hizo sharti yaandamanishwe na sababu zilizochangia kutolewa kwayo..

**TAREHE:** Februari 5, 2025.

**Dkt Peris Mang'ira, PhD, HSC**
Mkurugenzi wa Kitaifa wa Mpango wa Miji
**Idara ya Serikali ya Kitaifa kuhusu Ardhi na Mpango wa Miji**